

**BENKI KUU YA TANZANIA**

16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
Simu: 255 22 223 3167
Barua pepe: botcommunications@bot.go.tz

BANK OF TANZANIA

16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
Phone: 255 22 223 3167
Email: botcommunications@bot.go.tz

18 Desemba 2023

TAARIFA KWA UMMA**KUFUTA LESENI YA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA DARAJA LA PILI YA MSILIKARE MICROFINANCE COMPANY LIMITED**

Kwa mamlaka iliyopewa kupitia kifungu namba 25(1)(b) na (e) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 pamoja na kanuni zake, Benki Kuu ya Tanzania imefuta leseni ya biashara ya huduma ndogo za fedha iliyotolewa kwa Msilikare Microfinance Company Limited kuanzia tarehe 15 Desemba 2023.

Uamuzi huu umechukuliwa baada ya Benki Kuu ya Tanzania kujiridhisha kuwa Msilikare Microfinance Company Limited imekua ikiendesha shughuli zake kinyume na:

- a) vigezo na masharti ya leseni ya biashara ya huduma ndogo za fedha; na
- b) matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 na kanuni zake.

Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuhakikisha kuwa maslahi ya watumiaji wa huduma ndogo za fedha yanalindwa kupitia uchunguzi wa ukuaji, upatikanaji na utumiaji wa huduma jumuishi za fedha.

GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA